

Nina weza aye kuleta familia yangu hapa?



Kuhusu Huduma ya Bakimbizi

Huduma ya Bakimbizi ni huduma ya yenye iko specialise ya Msaada ya Kisheria NSW. Mwakili wala Avocats wetu bana basaidia basaidiwa bakimbizi na jamii zenye matatizo kama vile uhamiaji wala immigration, nyumba, Centrelink, madeni, kuhachana na talaka. Huduma zetu ni za bure na za siri. Tazama page 14 jinsi ya kuwasiliana nasi. Kitabu hiki kinakuonyesha jinsi ya kutuma ombi wala demande ya kuleta familia yako Australia.

Ninaweza kuleta familia yangu ya bakimbizi Australia

wewe ni mkazi wala mtu alisha ikala miaka mingi Australia wala weye ni raia wa Australia, na:

- wewe ni mkazi wala mtu alisha ikala miaka mingi Australia wala weye ni raia wa Australia, na
- Familia yako:
 - iko inje ya nchi yao ya kuzaliwa, na
 - wanaogopa kuhumizwa wala mateso katika nchi yabo ya kuzaliwa , na
 - hakuna nchi inengine ambayo banaweza kuishi kwa usalama na kudumu.

Ikiwa familia yako bado iko katika nchi yabo ya kuzaliwa, unaweza kufanya ombi ya familia ya mgawanyiko ili kumfazili wala ku sponsoriser mume au muke yako, mutoto anayekutegemea au mzazi yako (ikiwa iko chini ya miaka 18). Tunakuambia maombi ya 'familia iliyogawanyika' ni nini ku page ya 11 wa kitabu hii.

Maombi ya visa ya mukimbizi inafanywa kwa Idara wala departement ya Mambo ya Ndani. Tunawaita Mambo ya Ndani katika kitabu hii.



Pata bitambulisho na picha za batu banaotaka kutuma ombi ya visa

Unahitaji:



- Photo moya passport ya kila mwanafamilia mwenye iko ku ombi
- Copies certifiées conformes za documents za identité wala bitambulisho byenye batu ya familia biko nabyo kwa mfano:



- Passport wala Pasipoti
- Certificat de naissance wala kitambulisho ya kuzaliwa
- Kitambulisho
- Documents za citoyenneté
- Certificat ya marriage
- Actes de décès wala vyeti bya kifo



Copie certifiée ina maana kwamba avocat wala wakili au mtu mwingine aliye ruhusiwa lazima aangalie document kama ni original kisha aandike kwenye document photocopié kwamba ni copie conforme ya kweli. Madocuments zinaweza kuwa certifiés nje ya nchi au Australia. Ikiwa ni vigumu kufanya hivo usijali Jumuisha copie ya document



Documents ambazo haziko mu Kiingereza zinahitaji kutafsiriwa. Documets zinaweza kutafsiriwa nje ya nchi au Australia



Ikiwa mwanafamilia hana document, wanahitaji kueleza kwa nini hawana document zozote. Huenda wamezipoteza, au kuziibiwa, au labda hawakuwahi kupewa document zozote katika nchi yao wenyewe. Hili sio shida lakini unahitaji tu kuelezea kwa nini hawana document. Hata kama hawana document, bado unaweza kutuma ombi ya visa



Ikiwa familia yako imeandikwa na HCR wala UNHCR, Msalaba Mwekundu, Hilali Nyekundu, au Shirika la Kimataifa ya Uhamiaji (IOM), unapaswa kupata copie ya usajili huo pia na uiweke pamoja na ombi.



Jaza fomu ya kuomba visa



Fomu unazohitaji ni:

Form	Nani anapashwa kusaini
Fomu 842	Familia yako nje ya nchi
Fomu 681	Wewe. Au, ikiwa familia yako ina jamaa wa karibu ambaye ni mkaaji wala mtu alisha ikaa miaka mingi Australia au raia wa Australia, mtu huyo.



Unaweza kupata fomu hizi kutoka:

<https://immi.homeaffairs.gov.au/form-listing/forms/842.pdf>

<https://immi.homeaffairs.gov.au/form-listing/forms/681.pdf>

Usitumikishe fomu za zamani.



Lazima ujaze fomu kwa Kiingereza. Ikiwa familia yako itaandika majibu yabo mu lugha yabo benyewe lazima majibu yatafsiriwe. Ikiwa Kiingereza yako ni ya kutosha, unaweza kufanya tafsiri hii mwenyewe. Huhitaji kupata tafsiri rasmi.





Ukila mtu mzima wa familia aandike habari kuhusu matatizo yabo katika nchi yabo



Ikiwa mtu mmoja tu ana shida, basi mutu huyo tu anahitaji kuandika habari. Taarifa iliyoandikwa ni hadithi ya matatizo ya familia yako katika nchi yabo ya asili, banaogopa nini katika nchi yabo, na kwa nini hawawezi kurudi salama.



Inaweza kuonekana wazi kwa nini hawangekuwa salama. Lakini ni muhimu kutoa maelezo kwa sababu Mambo ya Ndani hutumia taarifa hiyo ili kujua jinsi ya kuamua ombi kwa haraka na ikiwa utaipa familia yako visa



Banaweza kuandika taarifa katika lugha yabo na kisha kuitafsiri kwa Kiingereza. Unaweza kutafsiri mwenyewe. Huhitaji tafsiri rasmi.

Taarifa zinapashwa kusema:

Balikuwa na matatizo gani katika nchi yabo.

- Wakati matatizo ilianza
- Ni nini kiliwapata na ni nani aliyesababisha shida kwabo
- Wali umizwa aye
- Je, waliomba msaada kutoka kwa serekali au polisi mu nchi yabo? Ikiwa hawakuomba msaada, kwa nini?

Taarifa lazima:

- kuzungumza hasa juu yao, na si matatizo ya jumla katika nchi yabo, na
- toa maelezo zaidi ya majina, mahali na nyakati.

Wanayoogopa ingetokea ikiwa bangerudi katika nchi yabo.

Sehemu hii ya taarifa ni muhimu sana, haswa ikiwa bamekuwa nje ya nchi yabo kwa miaka michache. ni muhimu kwamba Mambo ya ndani ya nchi ielewe ni kwa nini wangukuwa katika hatari ya kupata shida kama wangu rudi

Ni lazima waeleze kila aina tofauti ya mashida inayoweza kutokea kwabo katika siku zijazo

Ikiwa wanaogopa zaidi ya jambo moja kutokea, lazima baeleze kila jambo ambayo inaweza kutokea.

Hii ni sehemu muhimu sana ya musambo yabo. Ikiwa hawataambia Mambo ya Ndani kitakachowapata ikiwa watarudi mu nchi yabo kwa undani zaidi inakuwa vigumu kupata visa. haitoshi tu kusema kwamba itakuwa vigumu kwabo kwa sababu hawana nyumba, au hawana pesa, au hawana kazi.

Nani ata waumiza.

Familia yako lazima itoe maelezo ya batu bote banaofikiri banaweza umizwa. Kwa mfano, ikiwa banaogopa shida kutoka kwa:

- kikundi ya bapiganaji au kidini, banahitaji kusema jina la kikundi
- batu binafsi, banahitaji kutaja majina yabo
- makundi machache tofauti au batu binafsi, banapashwa kubataja bote.

Kwa nini bataumizwa.

Misambo hizo pia zinahitaji kusema kwa nini batu hawa batataka kubaumiza. baseme ikiwa sababu zabo kuumizwa ni kwa sababu ya utaiifa yabo, kabila, dini, maoni ya kisiasa au sababu zinginezo

Ikiwa ni serikali ya nchi yabo ndiyo itakayowafanya vibaya, waseme kwa nini serikali itawafanya vibaya.



HATUA YA 4

Hakikisha kila kitu kiko sawa kabla ya kuituma kwa Mambo ya Ndani



Ukiweza, pata angalau taarifa zilizokaguliwa na Avocat wala wakili wa uhamiaji kabla ya kutuma fomu hizo kwa Idara ya Mambo ya Ndani

Huduma ya Wakimbizi katika Msaada wa Kisheria NSW inaweza kukupa ushauri wa kisheria bila malipo na wa kibinafsi lakini hatuwezi kuangalia fomu zako

Tunaweza kuzungumza naweye kuhusu unachohitaji kuweka katika msambo ili kujumuishwa na programu (Hatua ya 3) ili kuhakikisha kuwa umeweka kila kitu kinachofaa. Tazama page ya 14 kwa maelezo yetu ya mawasiliano na jinsi ya kupanga rendez vous ya kutuona

HATUA YA 5



Fanya macopies ya madocuments zote

Chunga copy ya ombi na ya documents zote zinazoenda na ombi.





Omba visa

Tuma maombi na documents kwa:



Department of Home Affairs
Special Humanitarian Processing Centre
(Departement ya Mambo ya Ndani)
GPO Box 9984 SYDNEY NSW 2001



Unaweza pia kutuma maombi ya visa hii mtandaoni lakini tu ikiwa kila mutu mwenye iko kwa ombi iko na picha wala photo ya passport ambayo anaweza kuambatisha kwa njia ya kielektroniki kwenye programu.



Nenda kwa <https://immi.homeaffairs.gov.au>

ikiwa utaamua kutuma ombi kwa mtandao, fuata maagizo ili kukamilisha ombi la mtandaoni na kupandisha fomu, documents na picha zako zilizojazwa. Kisha finya bouton ya 'Tuma'.



Liste ya contrôle

- Hatua 1:** Pata documents za bitambulisho na picha.
- Hatua 2:** Jaza fomu za kuomba visa.
- Hatua 3:** Mwombe kila mtu mzima wa familia aandike msambo.
- Hatua 4:** Angalia kama demande imekamilika na kila kitu kimeambatishwa kiko pamoja na demande.
- Hatua 5:** Fanya ma copies za documents zako zote.
- Hatua 6:** Omba visa kwa boite postale au kwa mtandao.



Ni nini demande 'ya famille divisée?



Unaweza kuomba kuleta mume yako, mke, partenaire au watoto wanaokutegemea (au ikiwa una umri ya chini ya miaka 18, bazazi yako) hadi Australia kupitia mpango wa famille divisee wala uliogawanyika ikiwa ulipewa visa ya mkimbizi, ya kibinadamu au ya ulinzi katika miaka mitano iliyopita, na:

1. Mume yako, mke, partenaire yako, batoto, au mzazi (ikiwa uko chini ya miaka 18) bado wanaishi katika nchi yabo ya asili, au banaishi nje ya nchi yabo, na
2. uliambia departement ya Mambo ya Ndani kuhusu familia yako KABLA ya kupata visa yako mwenyewe.

Kuomba visa ya aina hii, unatumia fomu zile zile (681 na 842), lakini unahitaji kusema ni ombi la 'famile divisee wala iliyogawanyika' kwenye Fomu 842

Kuna swali kwenye fomu inayouliza ikiwa hii ni maombi ya familje divisee wala iliyogawanyika na unahitaji kuweka tiki Ndiyo'

Kwa maombi hii, si lazima familia yako iandike taarifa yabo kuhusu kile kinachoweza kuwapata na kwa nini wao ni bakimbizi. Si lazima wathibitisha kuwa wao ni bakimbizi. Banahitaji tu kuthibitisha kuwa bana uhusiano na wewe, na kwamba uliwaambia departemenet ya Mambo ya Ndani (Home Affairs) kubahusu KABLA ya kupata visa yako mwenyewe.

Mambo ingine ya kujua



Itagharimu ngapi?

Hakuna kulipa kwa maombi ya visa. Ikiwa familia yako itapata visa, utalazimika kulipia tikiti za ndege ikiwa umefadhili. Wala ku sponsoriser.



Ni nini itatokea departement ya Mambo ya Ndani ikipata maombi hayo?

Batakutumia barua bakisema bamepata maombi. Barua hiyo itakuwa na namba ya fiche. Ni muhimu kuweka namba hii ya fiche kwa sababu ikibidi kufuatilia Mambo ya Ndani unahitaji kutumia namba hii ya fiche ili waweze kupata demande wala ombi.

Ikiwa hutapata barua ndani ya miezi mitatu, tuma barua ya email ku shp.enquiries@homeaffairs.gov.au ukiuliza kinachoendelea na ombi. Toa jina na tarehe ya kuzaliwa ya mwombaji katika barua ya email ili waweze kupata maombi.



?Itachukua muda gani?



Maombi yanaweza kuchukua miaka mingi - kwa ujumla kama miaka miwili.

?Je, familia yangu itapata visa?



Sio kila mtu atapata visa. Serikali inatoa idadi ndogo tu ya visa kila mwaka. Familia yako inaweza kukosa kupata visa.

Ikiwa una wasiwasi kuhusu inachukua muda gani

Una weza:

- uliza departement ya Mambo ya Ndani ikiwa ombi bado liko Australia au ikiwa wameituma kwa ubalozi ulio karibu na familia yako kwa ajili ya kushughulikiwa zaidi.
- Unaweza kupiga simu ku departement ya Mambo ya Ndani ku **13 18 81** au barua ya email ku shp.enquiries@homeaffairs.gov.au. Utahitaji namba ya fiche ili waweze kupata demande.
- wasiliana na Mbunge wa Jimbo lako (Mbunge) ikiwa imepitisha zaidi ya miezi 12 tangu utume fomu. Unaweza kumtafuta mbunge wa eneo lako kwa kuweka boîte postale unapoishi ku www.aph.gov.au/Senators_and_Members/Members



Utahitaji kuwaambia departemet ya Mambo ya Ndani ikiwa chochote kitabadilika

Ikiwa majibu yoyote ku maswali uliyotoa kwenye fomu yanabadilika, unahitaji kuwaambia departement ya Mambo ya Ndani.

Baadhi ya mabadiliko yanaweza kuwa kama:

- wewe au familia yako famille à l'étranger wala ugenini muli badilisha changez adresse wala anwani
- mtu mwenye iko katika maombi wala demende iko na mutoto, au
- familia yako inapokea vitisho bipya kutoka ku batu au bikundi byenye binataka kubadhuru.

Unaweza kuwaambia departement ya Mambo ya Ndani kuhusu mabadiliko yoyote kwa kuwatumia barua ya email ku shp.enquiries@homeaffairs.gov.au.



Muhimu! Unapashwa kuzungumza na wakili wa uhamiaji kabla ya kutumia habari hii ikiwa:

- ulikuja Australia na boti na uko na visa 866
- familia yako banaishi kwa usalama katika nchi ingine, au
- familia yako imekataliwa visa hapo zamani



Ninaweza kuona wapi avocat wala wakili?



Unaweza kupata usaidizi bila malipo kutoka kwa mwanasheria wala avocat katika Huduma ya ya Bakimbizi.

Number ya simu: **02 8713 6725**

Addresse Email: refugeeservice@legalaid.nsw.gov.au

Tunaweza pata muda ya kuzungumza nawewe ana kwa ana au kupitia simu.



Ikiwa unahitaji wa kugeuza lugha yaani interprete, piga simu 13 14 50, uliza lugha unayotaka kisha mpe namba ya Huduma ya Wakimbizi. Hii ni huduma ya bure.



Nini ya kuleta ku rendez vous yako?

- Passsport, ImmiCard au Titre de voyage
- Carte ya Huduma ya Afya ya Centrelink au carte ya Pension
- Carte ya kitambulisho ya Picha ya NSW
- Barua zozote kutoka ku Idara ya departement Mambo ya Ndani
- Macopies za maombi yoyote ya visa ambayo umetuma kwa familia yako



Ikiwa unahitaji ku kata rendez vous yako

Ikiwa hutaweza kuja ku rendez vous, wasiliana na Huduma ya Bakimbizi ku 02 8713 6725 ili utufahamishe haraka uwezavyo.

Ninaweza kupata wapi habari zaidi?



Unaweza kupata taarifa zaidi kuhusu mpango ya bakimbizi na ya kibinadamu ya Australia katika www.homeaffairs.gov.au.



Publication hili ni mwongozo ya jumla ya sheria. Hupaswi kutegemea kama ushauri ya kisheria, na tunapendekeza kwamba uzungumze na wakili wala avocat kuhusu hali yako

Taarifa iko sawa wakati wa uchapishaji, hata hivyo inaweza kubadilika. Kwa maelezo zaidi wasiliana na LawAccess NSW kwa 1300 888 529.

This brochure is available in Arabic, Dari/Farsi, Burmese and English.



© Legal Aid Commission of NSW 2024

Agiza brochures mtandao kwa: www.legalaid.nsw.gov.au/ways-to-get-help/publications-and-resources

Kwa habari zaidi, tembelea: www.legalaid.nsw.gov.au

Unahitaji usaidizi ili kuwasiliana nasi?



Ikiwa unahitaji interprete, piga simu kwa Huduma ya Utafsiri na Ukalimani wala ugeuzaji lugha (TIS) kwa 131 450 (9 asubuhi-5 jioni) na ulize LawAccess NSW.

Je ? Unaona ni vigumu kusikia au kuzungumza?



Iwapo wewe ni kiziwi, au una matatizo ya kusikia au kuzungumza, wasiliana nasi kupitia Huduma ya Kitaifa ya Usambazaji Relay (NRS). Uliza LawAccess NSW kwenye 1300 888 529.

